- (b) mtu huyo aliyehudumiwa awe ni mtu wa kaya yake au mtu ambaye daktari huyo anajukumu la kumwalia.

Ufafanuzi

3.-(1) Katika Sheria hii, ila, iwapo maelezo yahitaji vinginevyo-"shirika lilokubaliwa" maana yake ni' shirika lilokubaliwa na Waziri kwa mujibu wa ibara. ya 6 kwa ajili ya kuendesha hospitali ya mtu binafsi kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

"hospitali" maana yake m mahali popote panapotumiwa kwa ajili ya kutoa huduma ya matibabu kwa watu walioumia au watu wenye maradhi au wenye magonjwa, na maana hiyo ifahamike kuwa ni pamoja na zahanati, kituo cha afya ya wazazi na watoto, kiliniki inayotoa huduma kwenye gari au chombo cha aina nyingine yoyote kinachosafiri kila mara au kiliniki iliyoko mahali pa kudumu, na vile vile jengo lolote linalotumiwa kwa ajili ya kutoa huduma ya matibabu, iwe siku zote au mara moja;

"daktari wa Umma" maana yake ni daktari aliye katika utumishi wa Serikali;

Sura ya
409

"daktari" maana yake ni mtu ambaye ameandikishwa au amepewa leseni kwa mujibu wa, Sheria ya Madaktari na Waganga wa Meno, na anayeruhusiwa na Sheria hiyo kuendesha shughuli za madaktari;

" matibabu" ifahamike kwa maana ya kawaida ya neno hilo na vile vile ni pamoja na shughuli zinazotekelezwa na wataalamu zinazohusika na uganga wa meno, kupasua wagonjwa, uzalishaji wa akina mama waja wazito, uuguzi, utoaji wa madawa, ushauri juu ya afya na utoaji wa huduma ya namna nyingine yoyote katika hospitali au utoaji wa vifaa vyovyote vinavyohusika na lolote kati ya mambo yaliyotajwa katika tafsiri hii, lakini maana hiyo isifahamike kuwa ni pamoja na shughuli za uganga wa wanyama;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya mambo yanayohusika na huduma, za utabibu na afya;

"shirika" ifahamike kwa maana ya kawaida ya neno hilo na vile vile ni pamoja na chama, ushirika au kikundi chochote cha watu, na

ni mambo kama kikundi hicho kimeandikishwa kama shirika kwa mujibu wa Sheria au sivyo, na vile vile maana hiyo ifahamike kuwa ni pamoja na mtu mmoja anayetambuliwa kuwa ni shirika kwa mujibu wa Sheria inayotumika kuhusu mashirika;

"hospitali ya mtu binafsi" maana yake ni hospitali yoyote isiyo hospitali ya Umma;

"hospitali ya Umma" maana yakea ni hospitali ya aina yoyote kati ya aina hizi zifuatazo, yaani-

- (a) hospitali ya Chama cha Mapinduzi au hospitali ya jumuiya yoyote iliyoshirikishwa na Chama cha Mapinduzi;
- (b) hospitali ya Serikali;
- (c) hospitali ya shirika lolote linalomilikiwa na Serikali au ya kampuni yoyote inayomilikiwa na Serikali, ama kwa Serikali kumiliki hivyo peke yake au kwa kushirikiana na shirika lolote au na kampuni yoyote, au hospitali ya shirika dogo la shirika kubwa linalomilikiwa na Serikali kwa namna hiyo iliyoelezwa awali au ya kampuni ndogo ya kampuni kubwa inayomilikiwa na Serikali kwa namna hiyo iliyoelezwa awali;
- (d) hospitali ya mtu binafsi yoyote ambayo baadhi ya mahitaji yake hupatikana kama msaada kutoka na na mali ya Umma au ambayo matumizi yake yote au sehemu ya matumizi yake hupatikana kama msaada kutokana na fedha ya Umma;
- (e) hospitali inayomilikiwa na idara yoyote ya Jumuiya ya Afrika Mashariki au na shirika lolote la Jumuiya hiyo, au hospitali inayomilikiwa na shirika lolote jingine la kimataifa ambalo Jamhuri ya Muungano ni mwanachama wake;
- (f) hospitali yoyote nyingine ambayo Waziri ataitaja na kuitangaza katika *Gazeti la Serikali* kuwa ni hospitali ya Umma kwa madhumuni ya Sheria hii.

(2) Kwa madhumuni ya kuwawezesha watu kuzitambua hospitali za watu binafsi za mashirika yaliyokubaliwa na hospitali za Umma, Waziri aweza kutoa maagizo kwa maandishi kwamba kila hospitali ya watu binafsi itambulishwe kwa, namna yoyote itakayoelezwa na Waziri katika maagizo hayo, na kila shirika lililokubaliwa linalohusika litatakiwa kutimiza maagizo hayo.

(3) Kanuni zifuatazo zitatumika katika ufafanuzi au utekelezaji wa masharti ya Sheria hii, yaani-

- (a) mtu atahesabiwa kuwa kuwa anaendesha hospitali ya mtu binafsi iwapo kwa niaba yake mwenyewe au kwa niaba ya mtu mwingine yeyote anatoa matibabu katika hospitali kwa mtu yeyote, kwa malipo, au anawaelewesha watu kwamba yuko tayari na anaweza kutoa matibabu katika hospitali kwa mtu yeyote, kwa malipo;
- (b) mtu atahesabiwa kuwa amepewa matibabu katika hospitali ya mtu binafsi bila ya kujali kama matibabu hayo amepewa yeye peke yake au pamoja na watu wengine kwa, wakati mmoja na vile vile bila ya kujali kama amepata matibabu hayo mara moja tu au zaidi ya mara moja;

- (c) iwapo eneo lote la mahali panapotumiwa kama hospitali ya mtu binafsi au eneo lote la majengo yanayotumiwa kwa ajili ya hospitali ya mtu binafsi limtumiwa kama ni eneo la hospitali moja, basi eneo hilo lote litahesabiwa kuwa na hospitali moja tu, bila ya kujali kama eneo hilo limeandikishwa katikia hati za kumiliki ardhi mbili au zaidi, hivyo, maana ya neno "hospitali" inabidi ifahamike kwa mujibu huo.

SEHEMU YA PILI

UTEUZI WA WATENDAJI NA MASHARTI KUHUSU UENDESHAJI WA HOSPITALI ZA WATU BINAFSI

Uteuzi wa Msajili na Wasaidizi wake

4.-(1) Waziri atamteua mtumishi wa Serikali kuwa Msajili wa Hospitali za Watu Binafsi na aweza kuteua idadi yoyote anayoona inafaa ya watumishi wengineo wa Serikali kuwa Wasajili Wasaidizi wa, Hospitali za Watu Binafsi.

(2) Msajili atafanya kazi na kutekeleza shughuli zilizotajwa katika Sheria hii kuwa ni kazi na shughuli za Msajili na pia atafanya kazi na kutekeleza shughuli nyinginezo zozote atakazoagiza Waziri au ambazo Waziri atazitaja katika Kanuni atakazoweka kwa mujibu wa Sheria hii.

(3) Kila Msajili Msaidizi atamsaidia Msajili katika utendaji wa kazi na shughuli zake kwa mujibu wa Sheria hii na, kwa, kufuata uongozi na usimamizi wa Msajili, Msajili Msaidizi aweza kufanya kazi au kutekeleza shughuli yoyote ya Msajili.

Masharti kuhusu uendeshaji wa hospitali za watu binafsi

5. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuendesha hospitali ya mtu binafsi au kumruhusu mtu mwingine kuendesha hospitali ya mtu binafsi, ila kwa niaba ya shirika lililokubaliwa.

(2) Ni marufuku kwa shirika lolote kuendesha hospitali ya mtu binafsi, ila kama shirika hilo liwe ni shirika lililokubaliwa na hiyo hospitali iwe imeandikishwa kwa mujibu wa Sheria hii.

(3) Mtu yeyote atakayetenda kinyume cha masharti ya ibara ndogo ya (1) au ya ibara ndogo ya (2) atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia mbele ya mahakama atapaswa kuadhibiwa kwa kutozwa faini isiyozidi shilingi laki moja au kufungwa gereza kwa muda, usiozidi miaka mitano au kupewa adhabu hizo zote mbili pamoja.

Uwezo wa Waziri wa kuyakubali mashirika

6.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (3), baada ya kupokea maombi, Waziri aweza kutoa kibali au kutoa kibali upya cha kulikubali shirika lolote linalostahili kukubaliwa kwa mujibu wa ibara ndogo ya (2) ili shirika hilo liendeshe hospitali ya mtu binafsi.

(2) Shirika litastahili kukubaliwa kwa mujibu wa ibara hii iwapo tu linatimiza masharti yafuatayo, yaani-

- (a) madhumuni ya shirika yawe ni shughuli za kuendeleza dini; au
- (b) shirika liwe limeundwa kwa madhumuni ya kuinua hali ya maisha ya wafanyakazi au wakulima; au
- (c) shirika liwe linatekeleza shughuli nyingine yoyote inayoleta au kuendeleza masilahi ya Umma.

(3) Wazari hana madaraka ya kulikubali shirika lolote kwa mujibu wa ibara hii iwapo shirika hilo linatekeleza au linakusudia kutekeleza shughuli yoyote inayohusika na uendeshaji wa hospitali ya mtu binafsi yoyote kwa madhumuni ya kutimiza jambo lolote kati ya mambo yafuatayo, yaani-

- (a) kupata faida; au
- (b) kuendeleza masilahi ya kiuchumi ya wanachama wa shirika hilo; au
- (c) kusaidia utekelezaji bora au kurahisisha. utekelezaji wa shughuli za shirika jingine lolote linalotekeleza shughuli zenye lengo la kuleta faida au kuendeleza masilahi ya kiuchumi ya wanachama wake.

(4) Waziri aweza kukataa kutoa kibali au kutoa kibali upya kwa mujibu wa ibara hii kwa ajili ya shirika lolote bila ya kutoa, sababu zozote za kukataa kwake.

(5) Maombi ya kumtaka Waziri atoe kibali au atoe kibali upya, yatapelekwa kwa Waziri kwa maandishi na yatataja jina na anwani ya shirika linalopeleka maombi, hospitali inayohusika na maombi hayo na yatatoa maelezo mengineyo, yoyote yatakayotakiwa kwa mujibu wa Kanuni zitakazowekwa kwa mujibu wa Sheria hii.

(6) Kanuni zifuatazo zitatumika kwa kila kibali kitakachotolewa na Waziri kwa mujibu wa ibara hii, yaani-

- (a) kibali kitatolewa kwa hati iliyoandikwa au kutiwa sahihi na Waziri, na kitatolewa bure;
- (b) kibali kitatumika kwa muda wowote utakaotakiwa na Waziri, na muda huo ukimalizika, Waziri aweza kutoa kibali upya, lakini Kanuni hii itatumika bila ya kuathiri masharti ya, ibara, ya 8;
- (c) shirika lililopewa kibali halitaruhusiwa kuazimisha kibali chake kwa shirika jingine lolote.

7.-(1) Msajili ataweka daftari maalum atakamoandika jina la kila shirika lililokubaliwa na pia maelezo, mengineyo yoyote juu ya shirika hilo anayoona yanafaa kuandikwa katika daftari hilo, na kila inapohitajia atafuta au atasahihisha maelezo hayo.

(2) Kila mwaka Msajili atatangaza angalau mara moja katika *Gazeti la Serikali* au katika gazed lolote linaalosambazwa, nchini kote orodha, ya mashirika yaliyokubaliwa yote ambayo vibali vyake bado vinatumika.

(8). Wakati wowote Waziri aweza kubatilisha kibali chochote kilichotolewa kwa mara ya kwanza au kilichotolewa upya, kwa mujibu wa ibara ya 6, kwa sababu yoyote kati ya sababu ziuatazo yaani-

- (a) kwamba, shirika linalokubaliwa limekoma kuwa shirika linalostahili kukubaliwa kwa mujibu wa ibara ya 6 (2); au
- (b) kwamba shirika, lilokubaliwa, linaendesha hospitali ya shirika kwa, madhumuni ya kutimiza jambo moja au zaidi kati ya mambo yaliyotajwa, katika. ibara ya, 6 (3); au
- (c) kwamba, shirika lilokubaliwa halifai tena, kuendesha hospitali ya shirika.

Uandikishaji na utangazaji wa maelezo ya mashirika yaliyokubaliwa

Kubatilishwa kwa kibali

SEHEMU YA TATU

UANDIKISHAJI WA HOSPITALI ZA WATU BINAFSI

Uandikishaji
wa hospitali
za watu
binafsi

9.-(1) Ni marufuku kwa shirika lililokubaliwa lolote kuendesha hospitali ya mtu binafsi ila mpaka hospitali hiyo iwe imeandikishwa kwa mujibu wa ibara hii

(2) Maombi ya kuandikisha hospitali ya mtu binafsi yatapelekwa kwa Waziri kwa maandishi ambayo yatataja hospitali inayohusika na maombi hayo, na kutoa maelezo mengine yoyote yatakayotakiwa kwa mujibu wa Kanuni zitakazowekwa kwa mujibu wa Sheria hii kuhusu maelezo ya hilo shirika lililokubaliwa au hospitali yenyewe.

(3) Kila hospitali ya mtu binafsi inayoendeshwa na shirika lililokubaliwa itaandikishwa pekee, yaani bila ya kuchanganywa katika hospitali ya mtu binafsi nyingineyo yoyote.

(4) Iwapo kutatokea mabadiliko yatakayosababisha hospitali ya mtu binafsi iliyoandikishwa kwa mujibu wa ibara hii kumilikiwa au kuendesha na, shirika jingine, basi uandikishaji wa awali wa hospitali hiyo utabatilika baada ya siku thelathini tangu siku ile yalipotokea mabadiliko hayo.

(5) Baada ya kupokea maombi ya kuandikisha hospitali ya mtu binafsi yatakayopelekwa kwake kwa mujibu wa ibara hii pamoja na ada ya uandikishaji (kama inatozwa), Waziri aweza kuyakubali au kuyakataa maombi hayo iwapo Waziri, atayakubali maombi, basi atamwagiza Msajili kuiandikisha hiyo hospitali ya mtu binafsi iliyotajwa katika maombi na kumpa hiyo mwombaji cheti maalum cha kuthibitisha uandikishaji wa hiyo hospitali, na Waziri aweza kutaja masharti yatakayoambatana na cheti hicho au aweza kuagiza kwamba cheti hicho kito-lewe bila ya masharti yoyote.

(6) Kila cheti cha uandikishaji wa hospitali ya mtu binafsi kilichotolewa kwa mujibu wa ibara hii kitatakiwa kiwekwe katika hospitali inayohusika mahali kinapoweza kuonekana kwa urahisi.

(7) Bila ya kuingiliwa uwezo aliopewa Waziri na ibara ndogo ya (5) wa kukataa kuyakubali maombi yaliyopelekwa kwake kwa mujibu wa ibara hii, Waziri aweza kukataa, kuyakubali maombi ya kuandikisha hospitali ya mtu binafsi kwa sababu yoyote kati ya sababu zifuatazo, yaani-

- (a) kwamba mwombaji si shirika lililokubaliwa au kwamba si shirika linalostahili kukubaliwa kwa mujibu wa ibara ya 6 (2); au
- (b) kwamba hospitali ya mtu binafsi iliyotajwa katika maombi haiko chini ya usimamizi wa daktari au mtu mwingine yeyote anayefaa kuendesha hospitali yoyote au hospitali ya aina iliyotajwa katika maombi; au
- (c) kwamba itakuwa ni kinyume cha masilahi ya Umma kuandikisha hospitali hiyo kwa sababu ya dosari lililoko katika hospitali hiyo kutokana na mahali ilipo, jinsi ilivyojengwa, nafasi zake za sehemu za kuhudumia wagonjwa, wafanyakazi wake au zana na vifaa vyake, au kwamba majengo yanayotumika kama sehemu ya hospitali hiyo yana dosari kama hizo.

(8) Mtu yeyote atakayeendesha hospitali ya mtu binafsi yoyote ambayo haikuandikishwa kwa mujibu wa Sheria hii au atakayeendesha hospitali ya mtu binafsi yoyote ambayo uandikishaji wake umefutwa au umebatilika kwa sababu nyingine yoyote, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia mbele ya mahakama atapaswa kuadhibiwa kwa kutozwa faini isiyoziidi shilingi elfu hamsini au kufungwa gerezeni kwa muda usioziidi miaka mitatu au kupewa adhabu hizo zote mbili pamoja.

10.-(1) Msajili ataweke, daftari maalum atakamoandika jina la kila hospitali ya mtu binafsi iliyokubaliwa na Waziri kuandikishwa kwa mujibu wa ibara ya 9 na pia maelezo mengineyo yoyote anayoona yanafaa kuandikwa katika daftari hilo kuhusu hospitali hiyo, kila inapohitajika atafuta au atasahihisha maelezo hayo.

(2) Kila mwaka Msajili atatangaza angalau mara moja katika Gazeti la Serikali au katika gazeti lolote linalosambazwa nchini kote orodha ya hospitali za watu binafsi zote zilizoandikishwa na ambazo uandikishaji wake bado unatumika.

11.-(1) Iwapo kuna sababu yoyote kati ya sababu zifuatazo inayohusika na hospitali ya mtu binafsi iliyoandikishwa, yaani-

- (a) kwamba majengo ya hospitali hiyo hayafai kuendelea kutumiwa kwa ajili ya hospitali kwa sababu yanawekwa katika hali ya uchafu au yanawekwa katika hali inayohatarisha afya ya watu; au
- (b) kwamba huduma za matibabu zinazotolewa kwa wagonjwa haziridhishi; au
- (c) kwamba shirika lililokubaliwa kuendesha hospitali hiyo limehindwa kutimiza masharti ya Kanuni zozote zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria hii kuhusu wafanyakazi wake, nafasi ya sehemu za kuhudumia wagonjwa au zana na vifaa vinavyopasa, kuwemo katika hospitali ya mtu binafsi au kwamba shirika limeshindwa kutimiza Kanuni zilizowekwa kima cha chini cha kiwango au ubora wa chakula kinachotosha au kinachofaa kwa wagonjwa waliolazwa hospitalini,

basi Waziri aweza kutoa taarifa kwa maandishi ya kulitaka shirika lililokubaliwa linaloendesha hospitali hiyo lirekebishe dosari zozote zilizotajwa na Waziri katika taarifa hiyo na litimize maagizo hayo kabla ya muda wowote utakaotajwa na Waziri katika taarifa hiyo.

(2) Iwapo shirika lililokubaliwa litashindwa kutimiza katika muda ibara ndogo ya (1), basi Waziri aweza kulitaka shirika hilo lिलieleze kama kuna sababu yoyote ya maana ya kuzuia kufutwa kwa uandikishaji wa hospitali hiyo na iwapo shirika hilo litashindwa kabisa kujieleza au litatoa sababu isiyo ya maana, basi Waziri aweza kufuta uandikishaji wa hospitali.

SEHEMU YA NNE

USIMAMIZI juu YA VIWANGO VYA ADA ZINAZOTOZWA KATIKA HOSPITALI ZA WATU BINAFSI KWA AJILI YA MATIBABU

A: Katika Sheria hii, neno "ada" linapotumika kuhusu matibabu, maana yake ni malipo yoyote yanayotowazwa katika hospitali ya mtu binafsi yoyote kwa ajili ya matibabu aliyopewa mtu yeyote.

Wajibu wa Msajili kuhusu hospitali zilizoandikishwa

Kufutwa kwa uandikishaji wa hospitali

Ufafanuzi wa "ada"

Uwezo wa
Waziri wa
kuweka
viwango vya
ada

13.-(1) Waziri aweza, mara kwa mara, kuweka, kwa mujibu wa Sheria hii, viwango vya ada zitakazotowwa na, hospitali za, watu binafsi kwa ajili ya, matibabu yanayotolewa na hospitali hizo, na, aweza kuweka viwango hivyo ili vitumike katika, nchi nzima au katika sehemu maalum za nchi, na Waziri aweza, pia, kwa mujibu wa Sheria; hii, kufikiria tena viwango hivyo na kuvibadlilisha kila inapohitaiika.

(2) Katika kutumia uwezo aliopewa na ibara ndogo ya (1) wa, kuweka viwango vya ada kwa ajili ya matibabu, Waziri aweza pia kuweka kima, cha juu kabisa. cha ada kwa ajili ya aina yoyote ya, matibabu yanayotolewa. katika hospitali za, watu binafsi na aweza pia. kueleza jinsi hicho kima, cha juu cha ada. kitakavyopangwa na. kudhihirishwa.

(3) Wakati wa kuweka kima. cha ada, kwa ajili ya aina yoyote ya matibabu Waziri atazingatia mambo yafuatayo, yaani-

- (a) aina za matibabu ya lazima. kwa wananchi yanayopatikana. katika hospitali za watu binafsi na katika hospitali za Umma;
- (b) haja ya kupukana na hali ya kuwa na mabadiliko ya haraka au ya. mara kwa mara. ya. kima, cha ada;
- (c) haja ya kudumisha ubora, wa huduma zinazotolewa katika hospitali za watu binafsi;
- (d) haja ya kuziwezesha hospitali za watu binafsi kuendelea kutoa huduma bora na kupanua shughuli zake ili zisaidie huduma zinazopatikana katika hospitali za umma;
- (e) haja ya kuhakikisha, kwamba, huduma za matibabu na, za afya kwa jumla zinapatikana, katika sehemu za mijini na pia katika sehemu za vijijini.

(4) Zaidi ya mambo yaliyotajwa katika, ibara ndogo ya (3), wakati wa kuweka kima, cha, juu cha ada, kwa ajili ya matibabu, Waziri atafikiria gharama, za vifaa, (kama vimetumiwa), gharama za huduma yenyewe na viwango vya ushuru au kodi zinazotowwa hospitali za watu binafsi na mambo mengineyo yoyote ambayo waziri anaona. inafaa kuyafikiria.

(5) Katika kutumia uwezo wake kwa mujibu wa ibara hii, Waziri atakuwa na uwezo pia wa-

- (a) kupokea na kufikiria maombi kutoka mashirika yaliyokubaliwa ya kutaka Waziri aweke kuna cha juu cha ada au abadilishe kima cha juu cha ada;
- (b) kupokea na kufikiria maombi kutoka kwa mtu yeyote au shirika lolote au idara yoyote ya Serikali ya kutaka Waziri afikirie jambo lolote linalohusika na ada;
- (c) kuipelekea idara yoyote ya Serikali maelezo juu ya jambo lolote linalohusika na ada za matibabu ili apate ushauri juu ya jambo hilo kutoka idara hiyo;
- (d) bila ya kujaji masharti ya Sheria yoyote, kuagiza kwamba apatiwe maelezo juu ya jambo lolote linalohusika na huduma ya matibabu kutoka kwa mtu yeyote au shirika lolote au idara yoyote ya Serikali.

(6) Waziri aweza kutoa taarifa kwa maandishi ya kulitaka shirika lililokubaliwa lolote linaloendesha hospitali ya watu binafsi liwasilishe kwake, kabla ya kumalizika muda atakaotaja Waziri katika taarifa hiyo, mambo yafuatayo, yaani-

- (a) vitabu vya hesabu na kumbukumbu nyinginezo zinazohusika na uendeshaji wa hospitali hiyo;
- (b) maelezo ya mapato yaliyotolewa na hilo shirika lililokubaliwa kwa idara ya kodi kwa ajili ya makadirio ya kodi ya mapato au kodi ya aina nyingineyo yoyote iliyopata kulipwa na shirika hilo katika mwaka wowote;
- (c) habari nyinginezo zozote ambazo Waziri ataona inafaa kuzijua.

14. Hakuna mahakama yoyote itakayokuwa na mamlaka ya kuchunguza uamuzi wo wote uliotolewa na Waziri kwa mujibu wa Sheria hii kuhusu ada za matibabu.

15.-(1) Iwapo Waziri ameweka kima cha juu cha ada kwa ajili ya aina yo yote ya matibabu, basi Waziri atatoa taarifa itakayoeleza aina wa ya matibabu inayohusika na kima cha juu cha ada kilichowekwa kwa , ajili ya aina hiyo ya matibabu.

(2) Taarifa iliyotolewa kwa mujibu wa ibara ndogo ya (1) yaweza kutangazwa kwa namna yo yote ambayo Waziri anaona inafaa, ili mradi ahakikishe kuwa yaliyomo katika taarifa hiyo yatawafikia watu wanaohusika nayo.

(3) Tangu siku itakapotangazwa taarifa yo yote iliyotolewa kwa mujibu wa ibara hii au kuanzia siku nyingine yo yote ya baadaye iliyotajwa katika taarifa hiyo, kima cha juu cha ada kwa ajili ya aina ya matibabu yaliyoelezwa katika taarifa hiyo kitakuwa ndicho kima cha ada kitakachotumika kwa ajili ya aina hiyo ya matibabu.

(4) Mtu ye yote atakayetoa matibabu katika hospitali ya watu binafsi yo yote na kutoza ada inayozidi kima cha juu cha ada kilichowekwa kwa ajili ya aina hiyo ya matibabu, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia mbele ya mahakama atapaswa kuadhibiwa kwa kutozwa faini isiyozidi shilingi elfu kumi na tano au kufungwa gereza kwa muda usiozidi miaka mitatu au kupewa adhabu hizo zote mbili pamoja.

16.-(1) Waziri aweza kutoa amri, ambayo itabidi itangazwe katika *Gazeti la Serikali*, ya kulitaka shirika lililokubaliwa lo lote linaloendesha hospitali ya watu binafsi liweke katika hospitali inayohusika, na mahali inapoweza kuonekana kwa urahisi na wagonjwa, orodha ya vima vya juu vya ada vinavyotumika kwa ajili ya aina zote za matibabu zilizotajwa katika hiyo amri ya Waziri.

(2) Amri iliyotolewa kwa mujibu wa ibara hii yaweza kueleza jinsi hiyo orodha ya vima vya juu vya ada inavyotakiwa, kutengenezwa na kupangwa.

(3) Mtu ye yote anayehusika na uongozi katika, uendeshaji wa hospitali ya watu binafsi yo yote atakayekosa kuweka katika hiyo hospitali orodha ya vima vya juu vya ada vilivyowekwa kwa ajili ya matibabu atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia mbele ya mahakama atapaswa kuadhibiwa kwa kutozwa faini isiyozidi shilingi elfu tano au kufungwa gereza kwa muda usiozidi miezi kumi na mbili au kupewa adhabu hizo zote mbili pamoja.

Uamuzi wa waziri hautaingiliwa na mahakama Utangazaji wa viwango vya juu vya ada

Namna ya kuonyesha viwango vya juu vya ada

Utunzaji wa vitabu vya hesabu na kumbukumbu nyinginezo

17.-(1) Kila shirika, lililokubaliwa, linaloendesha hospitali ya watu binafsi inayotoa matibabu ambayo yamewekewa, kima. cha. juu cha. ada kwa mujibu wa Sheria, hii litaweka vitabu vya, hesabu au kumbukumbu nyinginezo kwa. ajili ya, matibabu yanayotolewa, na. shirika, hilo litaaandika, katika. vitabu hivyo au kumbukumbu hizo mambo yatakayotakiwa. yaandikwe humo kwa kufuiata, Kanuni zitakazowekwa kwa mujibu wa. Sheria. hii.

(2) Kila shirika lililokubaliwa, baada, ya kumaliza kuandika. kitabu cha, hesabu chote kinachotakiwa. kiwekwe kwa, mujibu wa, ibara. hii au baada ya kumaliza kuandika kumbukumbu yote inayotakiwa. iweke kwa, mujibu wa, ibara hii, litatunza kitabu hicho au kumbukumbu hiyo kwa muda wa, miaka miwili au kwa muda, mrefu zaidi kadri itakavyoelezwa katika Kanuni zitakazowekwa kwa, mujibu wa Sheria, hii.

Utoaji wa stakabadhi za malipo ya ada

18.-(1) Kila. mtu anayehusika, na. uongozi katika. uendeshaji wa hospitali ya, watu binafsi inayotoa kwa. mtu yeyote matibabu ambayo yamewekewa. kima, cha. juu cha, ada kwa. mujibu wa, Sheria hii, na matibabu ambayo yamelipiwa, au yatalipiwa ada, atatakiwa, kumpa huyo mtu aliyetibiwa, mapema; iwezekanavyo baada ya, matibabu, stakabadhi au hati ya deni la ada, ambayo itaeleza. aina, ya, matibabu yaliyotolewa na ada iliyolipwa au inayodaiwa kwa. ajili ya matibabu, hayo.

(2) Kila, mtu atakayetoa. stakabadhi au hati ya deni kwa, mujibu wa ibara hii atatakiwa. aweke katika. kumbukumbu za. hiyo hospitali nakala ya hiyo stakabadhi au hati ya. deni la ada.

(3) Mtu yeyote anayehusika na uongozi katika, uendeshaji wa hospitali ya. watu binafsi atakayekosa. kutimiza. masharti ya ibara. ndogo ya. (1) au ya, ibara. ndogo ya, (2), atakuwa ametenda, kosa. na, akipatikana, na, hatia mbele ya. mahakama atapaswa. kuadhibiwa kwa, kutozwa faini isiyozidi shilingi elfu tano au kufungwa. gerezeni kwa, muda usiozidi miezi kumi na mbili au kupewa. adhabu hizo zote mbili pamoja.

SEHEMU YA TANO

USIMAMIZI JUU YA VIWANGO VYA MISHAHARA YA MADAKTARI WAFANYAO KAZI KATIKA HOSPITALI ZA WATU BINAFSI

Usimamizi juu ya viwango vya mishahara ya madaktari

19.-(1) Iwapo Waziri ataona wakati wowote kuwa masilahi ya umma yahitajia kwamba inafaa uwepo usimamizi juu ya viwango vya mishahara wanayolipwa madaktari wanaofanya kazi katika hospitali za watu binafsi, au kwamba inafaa viwango vya mishahara hivyo vichunguzwe, basi Waziri aweza kuweka au kuchunguza viwango hivyo kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

(2) Katika kutumia uwezo aliopeva na ibara ndogo ya (1), Waziri atakuwa na uwazo pia wa kuweka kima cha juu kabisa cha mishahara halisi na vile vile kima cha juu kabisa cha posho na masilahi mengineyo (rnambo ambayo katika Sheria hii yataitwa kwa jumla "mishahara") wanayolipwa au wanayopata madaktari kwa, jumla au madaktari wa aina maalum yoyote kwa ajili ya huduma wanayotoa kwa mujibu wa mka. taba wa kazi au mapatano au mpango mwingineo wowote.

- (3) Wakati wa kuweka kima cha juu cha mishahara Waziri atazi-ngatia mambo, yafuatayo yaani-
- (a) tofauti zilizoko baina ya madaraka kwa jumla au kati ya madaktari wenye utaalum wa aina fulani maalum na ama nyingine au kati ya madaktari wa idara moja na wa idara nyingine katika shughuli za madaktari kuhusu elimu ya msingi ya udaktari, ujuzi wa kazi, maarifa katika utekelezaji wa kazi na kiasi cha madaraka ya utendaji;
 - (b) haja ya kudumisha na kuendeleza ustadi wa hali ya juu katika huduma zinazotolewa m madaktari;
 - (c) haja ya kuongeza na kudumisha idadi kubwa ya madaktari, wanaofanya kazi katika hospitali za watu binafsi;
 - (d) haja ya kuzuia tofauti kubwa kati ya mapato ya wananchi wanaofanya kazi za namna mbali mbali.
- (4) Katika kutumia uwezo wake kwa mujibu wa ibara hii, Waziri atakuwa na uwezo pia wa-
- (a) kupokea na kufikiria maombi ya kutaka aweke kima cha mishahara au abadilishe kima cha mishahara, lakini bila ya kuathiri masharti ya ibara ya 20 (3);
 - (b) kupokea na kufikiria maombi kuhusu mishahara ya madaktari kutoka kwa shirika lo lote au kutoka idara yo yote ya Serikali;
 - (c) kuipelekea idara yo yote ya Serikali maelezo juu ya jambo lolote linalohusika na mishahara ya madaktari ili apate ushauri juu ya jambo hilo kutoka idara hiyo;
 - (d) bila ya kujali masharti ya Sheria yo yote, kuagiza kwamba apatiwe maelezo juu ya jambo lo lote linalohusika na mishahara ya madaktari kutoka kwa mtu ye yote au shirika lo lote au idara yo yote ya Serikali.
- (5) Waziri aweza kutoa taarifa kwa maandishi ya kulitaka shirika lililokubaliwa lolote linaloendesha hospitali ya watu binafsi liwasilishe kwake, kabla ya kumalizika muda atakaoutaja Waziri katika taarifa hiyo, mambo yafuatayo, yaani-
- (a) maelezo kuhusu viwango vya mishahara ya madaktari wanaofanya kazi katika hospitali, ya watu binafsi inayoendeshwa na shirika hilo;
 - (b) maelezo kuhusu mapato ya fedha ambayo shirika hilo lategemea kupata katika mwaka wa hesabu wa shirika hilo na maelezo kuhusu jinsi fedha hiyo, inavyotazarniwa kupatikana;
 - (c) maelezo kuhusu makadirio ya matumizi ya shirika hilo katika mwaka huo wa hesabu wa shirika hilo.
- (6) Baada ya kupokea maelezo yaliyotajwa katika ibara ndogo ya (5), Waziri aweza kukubali bila ya mabadiliko viwango vya mishahara vilivyowasilishwa, kwake na hilo shirika au, akiona kwamba masilahi ya umma yahitajia afanye hivyo, aweza kutoa amri kwa maandishi ya kulitaka hilo shirika lirekebishe viwango vyake vya mishahara ili vilingane na vima vya juu vilivyotajwa katika amri yake, na kila shirika litakaloamriwa hivyo litatikiwa litimize maagizo hayo ya Waziri kabla ya kumalizika muda 'takaotajwa na Waziri.

(7) Kima cha juu cha mshahara kilichowekwa na Waziri kwa mujibu wa ibara ndogo ya (2) au ambacho kimekubaliwa au kimewekwa na Waziri kwa mujibu wa ibara ndogo ya (6) kitaitwa "mshahara wa haki", na kima hicho kitatiliwa nguvu kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

Utekelezaji
wa masharti
ya Sheria
kuhusu
viwango vya
juu vya
mishahara

20.-(1) Waziri atoa taarifa na kuitangaza katika Gazed la Serikali ambayo itakuwa na maelezo kuhusu kila mshahara wa haki uliowekwa au kukubaliwa naye kwa mujibu wa ibara ya 19, na pia maelezo ya vya aina ya madaktari watakaostahili kulipwa mshahara huo.

(2) Kanuni zifuatazo zitatumika kuhusu kila mshahara wa haki uliotangazwa katika *Gazeti la Serikali*, yaani-

- (a) hakuna mahakama yoyote itakayokuwa na mamlaka ya kuchunguza mshahara huo;
- (b) mshahara huo tu ndio utakaolipwa na waajiri au mashirika yaliyokubaliwa na ndio huo tu watakaostahili kupokea madaktari wote wanaohusika nao, na kanuni hii itatimizwa bila ya kujali masharti ya Sheria yoyote au mapatano ya mkataba wa kazi, mapatano mengineyo yoyote au ya mpango wowote mwingineo;
- (c) katika utekelezaji au ufafanuzi wa mkataba, mapatano au mpango wowote mwingineo baina ya waajiri au mashirika yaliyokubaliwa na madaktari itabidi ifahamike kwamba kuna lazima, kwa mujibu wa Sheria hii, ya kulipa au kupokea mshahara wa haki tu, hivyo masharti yote ya kazi yatakayotajwa kwenye huo mkataba au hayo mapatano au huo mpango yatatakiwa yatekelezwe kwa kufuata mshahara wa haki uliotangazwa mpaka hapo utakapo. badilishwa na kutangazwa tena katika *Gazeti la Serikali*.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote au shirika lolote kutoa maombi ya kutaka kubadilisha mshahara wa haki uliotangazwa katika *Gazeti la Serikali* kabla ya kumalizika miezi kumi na mbili tangu, siku ya kuanza kutumika mshahara huo, ila awe amepata kwanza ruhusa ya Waziri ya kutoa maombi hayo.

Utunzaji wa
kumbukumbu
kuhusu
malipo ya
mishahara

21. Kila shirika lililokubaliwa linaloendesha hospitali ya watu binafsi litaweka kumbukumbu za mishahara wanayolipwa madaktari wanaofanya kazi katika hospitali hiyo, na litatunza kumbukumbu hizo kwa muda wa Miaka miwili au kwa muda mrefu zaidi kadri itakavyoelezwa katika Kanuni zitakazowekwa kwa mujibu wa Sheria hii.

Marufuku
kufanya
mapatano
yenye lengo
la kuepa
masharti ya
Sheria hii

22. Tangu siku Bunge litakapopitisha Sheria hii, itakuwa marufuku kwa mwajiri yeyote au kwa shirika lolote kubadilisha au kurekebisha jambo lolote linalohusika na mshahara wa daktari lililotajwa katika mkataba, mapatano au mpango wowote mwingineo kwa madhumuni ya kuepa au kutengua masharti ya Sheria hii, na sharti hili litatimizwa bila ya kujali kama huyo daktari anayehusika amefiki au hakuafiki hiyo hatua ya kubadilisha au kurekebisha hilo jambo.

SEHEMU YA SITA
MASHARTI MBALI MBALI

23.-(1) Msajili wa Hospitali za Watu Binafsi, Msajili Msaidiizi wa Hospitali za Watu Binafsi, daktari wa umma, au mtumishi wa Serikali mwingine yeyote aliyeidhiniwa kwa maandishi na Waziri, akiwa na sababu ya kuamini kwamba matibabu yanatolewa katika jengo lolote linalotumiwa kama hospitali ya watu binafsi, aweza kumtaka mtu mwenye madaraka juu ya jengo hilo amruhusu aingie ndani na amsaidie kwa njia itakayomwezesha kuhakikisha kama matibabu hayo yanatolewa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii au kwa mujibu wa masharti ya kanuni zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria hii.

Ukaguzi na
upekuzi

(2) Iwapo mtumishi wa Serikali yeyote kati ya hao waliotajwa katika ibara ndogo ya (1), baada kuonyesha kitambulisho chake cha kazi kwa mtu yeyote atakayetaka kuhakikisha kwamba mtumishi huyo anayo mamlaka ya kukagua na kupekua, haruhusiwi kuingia katika hilo jengo au ikiwa anacheleweshwa au kusumbuliwa bila ya sababu ya maana, basi aweza kuingia katika jengo hilo hata kama hana hati maalum ya kumruhusu kupekua na aweza kukagua na kupekua kwa makusudi ya kuhakikisha mambo yale yaliyotajwa katika ibara ndogo ya (1).

(3) Mtu yeyote atakayemzuia au kumwekea vipingamizi huyo mtumishi wa Serikali katika utekelezaji wa wajibu wake kwa mujibu wa ibara hii, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia mbele ya mahakama atapaswa kuadhibiwa kwa kutozwa faini isiyozidi shilingi elfu tano au kufungwa gereza kwa muda usiozidi miezi kumi na mbili au kupewa adhabu hizo zote mbili pamoja.

24. Iwapo shirika lolote limetenda kosa lolote kinyume cha Sheria hii au kinyume cha Kanuni zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria hii, basi kila mtu aliyehusika katika uongozi wa shughuli za shirika hilo atakuwa pia ametenda kosa na atapaswa kushtakiwa na kuadhibiwa vilivyo, ila kama mtu huyo ataithibitishia mahakama kwamba hakujua kabisa kuwa kosa hilo lilikuwa linatendeka au kuwa lilikusudiwa au tilikuwa karibu kutendeka, au kwamba, alichukua hatua zote zinazofaa za kuzuia kosa lisitendeke.

Ufafanuzi wa
makosa
yanayotenda
na mashirika

25. Mabadiliko yafuatayo yanafanywa katika Sheria ya Madaktari na Waganga wa Meno, yaani-

Mabadiliko
katika Sheria
Sura ya 409

(a) katika ibara ya 2, ule ufafanuzi wa "mganga wa meno", "daktari" na "kutoa huduma ya matibabu" unafutwa na badala yake kutakuwa na ufafanuzi ufuatao: -

"mganga wa meno" maana yake m mtu mwenye ujuzi wa kutoa huduma ya uganga wa meno kwa wagonjwa;

"daktari" maana yake ni mtu mwenye ujuzi wa kutoa huduma ya matibabu kwa wagonjwa;

"kutoa huduma ya matibabu" maana yake ni shughuli zinazotekelezwa na madaktari zinazohusika na kupasua wagonjwa, utoaji wa madawa au ushauri juu ya afya, iwe huduma hizo zinatolewa mara moja au mara nyingi;"

(b) ibara ndogo ya (2) ya ibara ya 21 inafutwa;

(c) ibara yote ya 22 inafutwa.

Kanuni

26. Waziri aweza kuweka Kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa madhumuni na masharti ya Sheria hii, na bila ya kuathiri uwezo huo wa jumla, Waziri aweza, kuweka Kanuni kwa ajili, ya jambo lolote kati ya mambo yafuatayo, yaani-

- (a) kutengeneza fomu za namna mbali mbali zitakazotumiwa katika utekelezaji wa masharti ya Sheria hii.
- (b) kuweka viwango vya ada zitakazotoweka kwa ajili ya mambo yoyote yatakayotajwa katika Kanuni zitakazowekwa kwa mujibu wa ibara hii;
- (c) kuyaagiza mashirika yaliyokubaliwa kuwasilisha kwa Waziri mizania za hesabu zilizokaguliwa na pia kumbukumbu na maelezo mengineyo yanayohusika na mashirika hayo;
- (d) kuweka utaratibu wa kutekeleza masharti ya Sheria kuhusu viwango vya mishahara ya haki ya madaktari;
- (e) kutaja kiasi na aina ya chakula kinachofaa kupewa wagonjwa waliolazwa katika hospitali za watu binafsi; kupewa
- (f) kuyataka mashirika yaliyokubaliwa yanayoendasha hospitali za watu binafsi yaweke katika hospitali hizo vifaa na mahitaji mengineyo kwa ajili ya matumizi ya wagonjwa, ili wawe katika hali bora;
- (g) kutaja aina na idadi ya wafanyakazi wanaopasa, kuajiriwa katika hospitali za watu binafsi na pia kueleza, aina za nafasi na zana zinazofaa kwa ajili ya kutoa huduma, ya matibabu kwa wagonjwa;
- (h) kueleza jambo jingine lolote linalotakiwa au linaloruhusiwa kuelezwa kwa Kanuni kwa mujibu wa Sheria hii.

Masharti
yatakayo-
tumika
kwa muda

27.-(1) Wakati wowote baada ya kutungwa. Sheria hii, lakini kabla haijaanza kutumika, Waziri aweza kupokea na kufikiria maombi ya namna yoyote yanayotakiwa yawasilishwe kwake kwa mujibu wa Sheria hii na aweza kukata shauri juu ya maombi hayo kwa mujibu wa Sheria hii:

Isipokuwa kwamba iwapo Waziri atayakubali maombi yoyote kwa mujibu wa ibara hii, basi jambo hilo lililokubaliwa halitakelezwa mpaka siku itakapoanza kutumika Sheria hii au baada ya siku hiyo.

(2) Wakati wowote baada ya kuanza kutumika Sheria hii, lakini kabla ya kumalizika miezi sita tangu siku itakapoanza kutumika Sheria hii, Waziri aweza kutoa amri, ambayo itatakiwa Itangazwe katika *Gazeti la Serikali*, ya kuweka masharti ya nyongeza ambayo Waziri anaona yanafaa au yanahitajika kwa ajili ya kutilia nguvu au kurahisisha utekelezaji wa madhumuni na masharti ya Sheria hii.

Imepitishwa katika Bunge tarehe ishirini na nane Aprili 1977.



Katibu wa Bunge